BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Tisa – Tarehe 15 Mei, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2026/2027.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2026/2027.

III. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

427. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kwa kuwa kuna taratubu mbalimbali zimewekwa za kushughulikia namna ya kukamata wahalifu.

Je, utaratibu upi unaotumika wa kukamata wahalifu katika maeneo

tunayoishi kupitia Jeshi letu la Polisi.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

418. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa sasa mshahara wa Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi wa Wizara ama Idara ni tofauti na mshahara wa Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi wa Mashirika na Mamlaka, licha ya Vitengo vya Manunuzi vya Mawizara kuwa na kazi kubwa sana katika utekelezaji na usimamizi wa Miradi ya Kimkakati ya Serikali.

Ni lini Serikali itafanya mabadiliko ya maslahi ya wafanyakazi wa Kitengo hicho ambao wamepangiwa kazi mawizarani.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

14. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa kuwa Zanzibar ni nchi moja inayoundwa na visiwa vikubwa viwili vya Unguja na Pemba. Na kwa kuwa bandari ya Malindi Unguja na Mkoani Pemba zinasimamiwa na Serikali moja. Na kwa kuwa kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko ya wananchi wa visiwa hivi kulazimishwa kulipa ushuru wa bandari mara mbili, kwa kusafirisha vyombo vyao vya moto kutoka Unguja kwenda Pemba au kinyume chake.

Je, sababu gani ya msingi inayomfanya mwananchi wa nchi hii kulipa ushuru mara mbili (double taxation) kwa bidhaa ya aina moja kutoka bandari ya Malindi kwenda Mkoani Pemba au kinyume chake.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

101. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kama ilivyo kwa karafuu, zao la nazi ni moja ya zao la asili la kibiashara Zanzibar na alama kubwa katika visiwa vyetu. Hata hivyo, tofauti na karafuu, zao la nazi hivi sasa kama limetupwa, nazi zinaagizwa nje ya Zanzibar, huku kiwango cha kukata minazi kinaendelea kwa kasi na kutumika kwa shughuli za ujenzi na mashamba ya minazi kukatwa viwanja vya makaazi katika maeneo mbalimbali ya visiwa vyetu.

(a) Ni lini kwa mara ya mwisho imefanyika sensa ya minazi, ili kujuwa idadi ya minazi iliyobakia Zanzibar baada ya minazi mingi kukatwa.

(b) Je, hatua gani zinachukuliwa kulilinda na kuliimarisha zao la nazi Zanzibar, ili minazi isipotee visiwani.

(c) Je, ni miche mingapi inahitajika kuzalishwa kwa kila mwaka, ili kuimarisha zao la nazi Zanzibar.

<u>**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**</u>

388. MHESHIMIWA DKT. NASRA NASSOR OMAR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Walimu wa Chuo cha Ualimu Nkrumah walipangiwa kazi rasmi mwanzoni mwa mwezi wa Mei, wakati wanafunzi walitakiwa kuripoti Chuoni hapo, mwishoni mwa mwezi wa Septemba. Katika kipindi hicho, walimu waliendelea kutekeleza majukumu mbalimbali bila ya kulipwa stahiki zao.

(a) Je, kipindi ambacho walimu walikuwa wakifanya kazi bila ya kuwepo wanafunzi (Mwanzoni mwa mwezi Mei hadi Agosti), kinatambulika rasmi vipi kama ni muda wa kazi unaostahili malipo.

(b) Je, Serikali itawalipa lini walimu hao mishahara na posho zao zote walizokosa tangu walipoanza kazi.

<u>**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia na Habari ya Ubunifu:**</u>

377. MHESHIMIWA DKT. MAHMOUD OMAR HAMAD (Jimbo la Tumbatu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Lipo wimbi kubwa la matumizi yasiyo sahihi kwa mitandao ya kijamii na simu za mkononi ambapo udhalilishaji umeongezeka kupitia matumizi mabaya ya teknolojia hizo.

Je, kuna mpango gani wa kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii na simu za mikononi, ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza kwa jamii hasa watoto wadogo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

89. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Zao la mwani ambalo wakulima wake wengi ni akina mama katika maeneo ya ukanda wa pwani ikiwemo Micheweni Maziwa Ng’ombe, Paje, Jambiani, Kidoti na Nugwi, wamekuwa wakihangaika kupata soko la uhakika na bei nzuri. Pamoja na juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kuweka hali bora ya zao hilo, bado jitihada zaidi zinahitajika kuimarisha hali ya wakulima wa zao la mwani.

(a) Je, Serikali ina mipango gani hivi sasa ya kuwapatia ruzuku au kuondoa kodi zote katika zao la mwani, ili kuwasaidia wakulima wa mwani hasa akina mama kuongeza kipato.

(b) Je, katika kuimarisha uhakika wa soko, mpango wa Serikali wa kununua zao la mwani kama inavyofanya kwa karafuu, upoje.

(c) Hadi hivi sasa ni tathmini gani imefanyika kupata masoko mapya na kuimarishwa kwa bei ya mwani.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

282. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Mfanyakazi anaposimamishwa kazi ili uchunguzi ukamilike;

(a) Je, ni muda gani kisheria mfanyakazi anaweza kusimamishwa kazi.

(b) Iwapo uchunguzi haujakamilika, je, mfanyakazi huyo atapewa haki ya kurudishwa kazini au kufukuzwa kazi.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2026/2027.

Zanzibar,<br>15 Mei, 2026.

(Raya Issa Msellem)<br>KATIBU WA BARAZA LA<br>WAWAKILISHI, ZANZIBAR